# Jilinde dhidi ya ugojwa wa DONDAKOO

(DIFTHERIA)

## Chanjo ni ulinzi bora

**Chanjo ya diphtheria ni salama na bure kwa:**

- Watu walio chini ya umri wa miaka 20.
- Wanawake wajawazito kuanzia wiki 20.
- Watu wa Aboriginal na wa Torres Strait Islander ambao hawajapata chanjo ya diphtheria katika miaka 5 iliyopita.
- Watu wazima ambao hawajapata chanjo ya diphtheria katika miaka 10 iliyopita.
- Wakimbizi na wahamiaji wa kibinadamu.
- Wafanyakazi wa mstari wa mbele (huduma za afya)

Watoto huchanjwa mara kwa mara dhidi ya diphtheria kama sehemu ya ratiba ya chanjo ya NT.






**Je, huna uhakika kuhusu hali yako ya chanjo? Wasiliana na mtoa huduma wako wa afya!**

Ikiwa unahitaji mkalimani wakati wa kusoma hii, tafadhali muulize mfanyakazi.

NThealth

NORTHERN TERRITORY GOVERNMENT

# Je, Diphtheria ni nini?

**Diphtheria ni maambukizi ya ngozi au koo, yanayosababishwa na bakteria mbaya ambayo inaweza kukufanya kuwa mgonjwa sana na inaweza kuenea kwa wengine.**

## Kuna aina mbili za diphtheria:



### Diphtheria ya ngozi

Hii ndiyo aina ya kawaida na huathiri ngozi.

**Dalili:**

- Vidonda vya ngozi visivyopona na donda, hasa kwenye miguu.



### Diphtheria ya koo (kupumua)

Aina kali zaidi ya maambukizi ya diphtheria (dondakoo) iko kwenye koo.

**Dalili:**

- Maumivu ya koo, homa na baridi
- Ugumu kumeza na kupumua
- Mipako ya kijivu-nyeupe kwenye koo na tonsili
- Uvimbe, tezi zilizovimba na zenye maumivu kwenye shingo
- Uchovu, kutohisi njaa.

# Je, Diphtheria inaeneaje?

Bila matibabu, watu walioambukizwa wanaweza kueneza diphtheria kwa wengine.



Diphtheria huenezwa na matone yaliyoambukizwa kutoka kwenye kikohozi au kupiga chafya.

**KOHOA NA KUPIGA CHAFYA KWENYE KIWIKO CHAKO.**



Diphtheria inaweza kuenea kutokana na kugusana ngozi na kidonda kilichoambukizwa.

**WEKA MAJERAHA KATIKA USAFI NA VIFUNIKWE**



Unaweza kuugua kwa kugusa mashuka machafu, taulo, nguo, au vitu vya nyumbani.

**SAFISHA VITU VYA NYUMBANI NA NYUSO.**

# Matibabu

- Diphtheria inatibiwa na dawa za viuavijasumu ( antibiotics)
- Watu walio na maambukizi makali ya koo wanaweza kuhitaji matibabu hospitalini.

## CHANJO NI ULINZI BORA